

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKAL ZA MITAA
(TAMISEMI)



WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI
(TARURA)



MRADI WA UENDELEZAJI BONDE LA MSIMBAZI

Muhtasari Usio wa Kitaalamu: Mpango wa Uhamishaji wa Makazi &
Mpango wa Kuhuisha Njia za Kujikimu Kimaisha

Agosti 2026

Mradi wa Kuboresha Bonde la Msimbazi

Muhtasari Usio wa Kitaalamu: Mpango wa Uhamishaji wa Makazi & Mpango wa Kuhuisha Njia za Kujikimu Kimaisha

1. Mradi huu Unahusu Nini?

Mradi wa Kuboresha Bonde la Msimbazi ni mpango wa Serikali ya Tanzania, unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na wadau wengine, wenye lengo la kupunguza mafuriko makubwa na ya mara kwa mara yanayoliathiri Bonde la Chini la Msimbazi jijini Dar es Salaam. Bonde hilo lilitangazwa kuwa si salama kwa makazi ya binadamu tangu mwaka 1979 kutokana na hatari kubwa ya kutokea kwa mafuriko, lakini watu wengi wamekuwa wakihamia na kuishi hapo kwa miaka mingi. Mradi huu utajenga miundombinu kama vile matuta ya kuzuia mmomonyoko na mifereji ya maji ili kutatua changamoto hii. Ili kutekeleza mradi huu kwa usalama, watu wanaoishi na kufanya kazi katika maeneo hayo yaliyo hatarini kukabiliwa na mafuriko wanapaswa kuhamishwa.

2. Kwa nini ni Lazima Kufanya Uhamishaji?

Ujenzi wa miundombinu muhimu ya kukabiliana na mafuriko unahitaji utwaaji wa ardhi na utekelezaji wa kazi za ujenzi katika maeneo ambayo kwa sasa yanakaliwa na watu. Hii inamaanisha kuwa baadhi ya wakazi watatakiwa kuhama kabisa na kwenda maeneo salama zaidi, wakati wengine wanaoendesha biashara au kufanya shughuli za kilimo katika eneo hilo watapoteza mapato. Mpango huu umeandaliwa ili kuhakikisha mchakato huu unakuwa wa haki, wa wazi, na kwamba watu wanapata fidia inayostahili.

Mpango wa Uhamishaji wa Makazi (RAP) kwa ajili ya Eneo la Chini la Msimbazi umeandaliwa kwa ajili ya kutekelezwa katika awamu mbili; awamu ya kwanza ni kwa ajili ya eneo linalokumbwa na mafuriko na awamu ya pili ni kwa ajili ya miundombinu mingine inayohusiana ikiwa ni pamoja na ujenzi wa matuta ya kuzuia mmomonyoko. Utekelezaji wa Mpango huu wa Uhamishaji utafanyika kwa awamu ukianza na awamu ya kwanza ambayo inaendelea.

Msingi madhubuti wa Mpango wa Uhamishaji wa Makazi (RAP) na Mpango wa Kuhuisha Njia za Kujikimu Kimaisha (LRP) ni tafiti na uchunguzi wa hali iliyopo sasa, mahojiano na watu ambao kwa sasa wanaishi katika Bonde la Chini la Msimbazi, pamoja na uthamini wa mali na shughuli zinazochangia mapato na kujikimu kimaisha.

3. Ni watu Wangapi Wameathiriwa?

Mpango wa Uhamishaji wa Makazi (RAP) ya awamu zote mbili ya tarehe October 2023 unakadiria kuathiri moja kwa moja takriban kaya 5,966, kukiwa na jumla ya watu zaidi ya 12,000 kwa kujumlisha wanafamilia wote na wapangaji. Kati ya hawa:

- Kaya zaidi ya 2,500 zinakabiliwa na uhamishaji wa makazi, ikimaanisha kuwa zitahitaji kuhamisha nyumba zao kwenda maeneo mengine.
- Kaya 165 zinakabiliwa na uhamishaji wa kiuchumi, ikimaanisha kuwa zitapoteza chanzo cha mapato kama vile shamba, duka, au kibanda cha sokoni.
- Mradi huu pia utaathiri takribani majengo 2,800 na miti zaidi ya 5,100.

4. Walioathiriwa Watapata Nini?

Majengo

Fidia inakokotolewa kwa kuzingatia gharama ya uhamishaji, kwa maana ya kwamba watu wanalipwa kiasi cha kutosha kufidia kile wanachopoteza kwa bei ya sasa ya soko, bila ya makato yoyote. Stahiki mahususi zinategemea hali ya mtu na zimeainishwa kwa kina kwenye Jedwali la Stahiki katika Sehemu ya 6 hapa chini.

Uthamanishaji wa Ardhi

Ni muhimu kuzingatia kuwa uthamini wa ardhi ulihusu tu ardhi itakayotwaliwa kwa ajili ya matuta ya kuzuia mmomonyoko, na hivyo vipimo vya ardhi vilichukuliwa kwa wale Walioathiriwa na Mradi na wale watakaoguswa na ujenzi huo wa matuta pekee; wakati kwa wale waliopo eneo la Bonde la Chini la Msimbazi ambao hawana umiliki wa kisheria wa ardhi, vipimo havikuchukuliwa kwa kuwa Waathiriwa wa Mradi hao watapokea malipo ya kiwango sawa ili kuwasaidia kununua ardhi mahali pengine.

Ili kuhakikisha kuwa watu wasio na sifa hawapati nafasi ya kuwasilisha madai ya stahiki za fidia, tarehe ya ukomo iliwekwa, ambayo ni tarehe 10 Novemba 2021 kwa Mwathiriwa wa Mradi wa maeneo yanayokumbwa na mafuriko, na tarehe 14 Novemba 2022 kwa Mwathiriwa wa Mradi kutokana na kazi za ujenzi wa miundombinu. Tarehe ya ukomo maana yake ni tarehe ya kuanza kwa sensa na zoezi la kuhesabu mali.

5. Je Migogoro na Malalamiko Yatahughulikiwaje?

Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko (GRM) umewekwa ili mtu yeyote anayehisi kuwa ametendewa isivyo haki aweze kuwasilisha malalamiko yake. Kamati za malalamiko zinafanya kazi katika ngazi mbili: ngazi ya mtaa na ngazi ya wilaya. Kamati hizi zinajumuisha wawakilishi kutoka mashirika ya kijamii na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), ukijumuisha taratibu za kushughulikia masuala nyeti kama vile ukatili wa kijinsia. Lengo ni kutatua malalamiko kwa haraka, kwa haki, na kuwa karibu zaidi na jamii kadri inavyowezekana.

6. Jedwali la Stahiki

Jedwali la Stahiki linaainisha bayana kile ambacho kila kundi la Mwaathiriwa wa Mradi anastahili kupokea, kulingana na aina ya hasara au upotevu aliopata.

6.1 Upotevu wa Ardhi

Aina ya Mwathiriwa	Stahiki	Maelezo
Wamiliki halali (wanaomiliki rasmi kisheria)	Fidia ya fedha taslimu kuendana na gharama ya uhamishaji AU utoaji wa ardhi mbadala ya ukubwa na matumizi sawa. Posho ya usumbufu ya asilimia 7 ya thamani ya ardhi. Mradi utagharamia kodi za usajili/uhamisho wa umiliki na gharama za utoaji wa hatimiliki za ardhi.	Watu Walioathiriwa na Mradi wanaopokea Shilingi milioni 35 au zaidi na wanaweza kuchagua kubaki hapo hapo, kwenda karibu na eneo hilo, au mbali na eneo hilo. Waathiriwa wa Mradi wanaopokea chini ya Shilingi milioni 35 wanachagua fidia ya fedha taslimu au kupewa ardhi mbadala katika eneo la Mvuti.
Makazi yasiyopimwa (hawana haki ya umiliki lakini wanatumia ardhi)	Fidia ya fedha taslimu kwa ajili ya majengo/ujenzi kwa gharama inayoendana na uhamishaji. Posho ya usumbufu ya asilimia 7. Uhakika wa kupewa umiliki wa ardhi mbadala AU fedha taslimu kwa ajili ya kuwezesha kununua ardhi mbadala (mfano, Mvuti katika Wilaya ya Ilala). Wale walio na Ardhi pekee bila mali: Uhakika wa kupewa umiliki kwa ajili ya kufidiwa ardhi wanayotumia au/ Fedha taslimu kwa ajili ya kusaidia kununua ardhi mbadala kwa hiari katika eneo la Mvuti Wilaya ya Ilala.	Walioathiriwa na Mradi wanachagua kati ya fidia ya fedha taslimu au mbadala. Maeneo ya fidia ya ardhi mbadala ni pamoja na kuchagua kubaki hapo hapo, kwenda karibu na eneo hilo, au kwenda eneo la umbali wa zaidi ya kilomita 5 kutoka eneo la Jangwani.

Wavamizi wa hifadhi ya barabara chini ya TANROADS	Hakuna fidia kwa sababu walishapewa fidia na TANROADS hapo awali.	Haki ya kuokoa vifaa vyao vya ujenzi.
---	---	---------------------------------------

6.2 Hasara ya Jengo (Nyumba ya Kuishi)

Aina ya Mwathiriwa	Stahiki	Maelezo
Wamiliki wenye umiliki rasmi wa kisheria Njia ya pesa taslimu	Gharama ya ufidiaji + Posho ya malazi (miezi 36) + Posho ya usumbufu (hadi asilimia 7) + Posho ya usafiri (tani 20 hadi kilomita 20) + Haki ya kuokoa vifaa + Gharama za usajili na kodi zote za uhamisho wa umiliki. Posho ya Usafiriri a malazi ni kwa wale tu watakapo kutwa wanaishi eneo la mradi	Upotevu kamili unafasiliwa kama: kubomolewa kwa nyumba nzima, kupotea kwa zaidi ya asilimia 30 ya eneo lililoathiriwa, au kupotea kwa sehemu muhimu za nyumba (shimo la majitaka/choo/jikoni). Kiwango cha ukomo cha shilingi milioni 35 kinatumika kuamua katika kuchagua eneo la makazi mapya
Wamiliki wenye umiliki rasmi wa kisheria Njia ya malipo ya vitu mbadala Walioondolewa 2015/2016	Nyumba mpya yenye idadi sawa ya vyumba + miundombinu + posho za usumbufu na usafiri. Makazi mapya wa kiwango sawa.	Vigezo ni vilevile kama ilivyo hapo juu. Itatolewa fedha taslimu pekee kwa ajili ya kununua ardhi. Hakuna thamani ya jengo iliyotolewa hadi ilipofika tarehe ya ukomo.
Wapangaji (wa kuishi au biashara)	Kurejesha kiasi cha fedha kichobaki baada ya kulipia kodi ya kupanga/dhamana + Posho ya malazi (miezi 3 kwa kiwango kilichobadilika).	Uthibitisho wa upangaji unahitajika. Kiasi hicho kitatolewa kwenye fedha ya fidia kwa mwenye nyumba inayotolewa kufidia hasara ya ukosefu wa faida ya biashara.

6.3 Hasara ya Sehemu Muhimu za Majengo (mfano majiko, stoo, uzio)

Aina ya Mwathiriwa	Stahiki	Maelezo
Wamiliki	Fidia ya fedha taslimu kulingana na gharama ya uhamishaji kwa ajili ya upotevu mdogo au upotevu kamili. Posho ya usumbufu ya asilimia 7.	Inalenga majengo ambayo ni ya nyongeza kwa majengo ya makazi makuu.

6.4 Mazao ya Kuvunwa, Miti, na Mimea

Aina ya Mwathiriwa	Stahiki	Maelezo
Wamiliki, Wapangaji na Wavamizi	Fidia ya fedha taslimu kulingana na gharama ya zao. Posho ya usumbufu ya asilimia 7 ya jumla ya thamani ya mazao/miti. Haki ya kuvuna miti na mazao.	Mazao ya kudumu yanathaminiwa kulingana na wastani wa mavuno (kilo/mti/mwaka). Mradi lazima uzingatie mienendo ya upandaji mazao ili kuepuka Hasara za msimu.

6.5 Upotevu wa Njia za Kujikimu Kimaisha na Faida

Aina ya Mwathiriwa	Aina za Hasara	Stahiki
Wafanyabiashara na wamiliki wa biashara waliosajiliwa/wenye leseni	Upotevu wa faida wa kudumu au wa muda mfupi	Pesa taslimu: Kufidia hasara ya upotevu wa faida ya kila mwezi kwa

		kipindi cha miezi 36 + Posho ya usafiri. Kwa fidia mbadala: Msamaha wa kodi/malipo ya pango la biashara + Eneo jipya la biashara.
Waathiriwa wa Mradi kwenye maeneo yanayokumbwa na mafuriko mara kwa mara	Upotevu wa thamani halisi (ufikiwaji wa maeneo)	Uhakika wa umiliki ya ardhi katika eneo linalofaa AU kupewa ardhi mbadala au fedha taslimu kwa kiwango sawa.
Wafanyakazi waliosajiliwa/wenye leseni (masoko/machinjio)	Hasara ya kupoteza kipato kwa muda	Fidia ya fedha taslimu kwa kipindi cha kuvurugika kwa shughuli kulingana na faida halisi AU posho ya upotevu wa faida ya asilimia 7 kwa miezi 6 + Eneo mbadala la muda la kufanyia kazi.

6.6 Makundi yaliyo Hatarini

Aina ya Mwathiriwa	Stahiki	Maelezo
Waathiriwa wa Mradi walio katika mazingira magumu (kaya zinazoongozwa na wanawake au wazee, kaya zenye kipato cha chini, watu wenye ulemavu)	Misaada ya ziada ya kuongezea kwenye stahiki zote zinazohusu posho.	Hali ya kuwa kwenye hatari huthibitishwa wakati wa utafiti wa kijamii na kiuchumi. Msaada mahususi utatolewa kulingana na mazingira au hali ya mtu binafsi.

6.7 Upotevu wa Rasilimali za Pamoja

Aina ya Mwathiriwa	Stahiki	Maelezo
Watumiaji/wanajamii (visima, njia za kupita, vituo vya maji)	Urejesho au uhusishaji wa maeneo ya jamii yaliyoathiriwa.	Ufidiaji wa miundombinu kwa kutoa wmbadala wake kwenye maeneo yanayofikika.
Jumuiya za kidini (makanisa, misikiti)	Ubadilishaji au kujenga upya majengo ya ibada kwa kushauriana na jamii iliyoathiriwa.	Mwafaka kuhusu usanifu na eneo la miundombinu mbadala hufikiwa kupitia ushirikishwaji wa jamii.
Familia/wamiliki (makaburi na maeneo ya matambiko)	Gharama za ukarabati au uhamishaji kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania (Sheria ya Kuhamisha Makaburi ya Mwaka 1969). Gharama zitahusisha taratibu za kuzika upya, majeneza, na kujengea makaburi.	Process conducted with full respect for cultural and religious practices. Mchakato utakaotekelezwa kwa kuzingatia na kuheshimu kikamilifu tamaduni na misingi ya kidini.

6.8 Athari za Shughuli za Ujenzi

Aina ya Mwathiriwa	Aina ya Athari	Stahiki
Watumiaji wa mara kwa mara	Kupoteza njia	Kutoa njia mbadala za watu kupita (njia, vivuko vya mbao) zisizozidi urefu wa meta100
Wamiliki/watumiaji wa jengo	Uharibifu kwenye jengo (mipasuko au kuanguka) kutokana na shughuli za ujenzi.	Kuwa na Mpango wa ziada wa Uhamishaji wa Makazi kwa ajili ya fidia ya vitu mbadala au ya fedha taslimu kwa ajili ya jengo lililoharibiwa. Fedha taslimu kwa ajili ya posho ya malazi ya muda wa miezi 6 kufidia makazi yaliyoathirika vibaya zaidi.

7. Bajeti ya Jumla

Kipengele cha Bajeti	Makadirio ya Gharama (TZS)
Awamu ya 1 ya Fidia (ardhi, majengo, miti na posho)	70,658,282,945
Fidia ya Miundombinu Mengine	29,941,703,195
Utawala (ufuatiliaji, Kushughulikia malalamiko, ada ya uwakala)	1,800,000,000
Programu za Kuhusisha Njia za Kujikimu Kimaisha	917,999,999

8. Muhtasari

Mpango huu unahakikisha kuwa watu walioathiriwa zaidi na kazi za kuzuia mafuriko katika Bonde la Chini la Msimbazi wanatendewa haki, wanalipwa fidia stahiki inayoendana na gharama halisi za uhamishaji ya majengo na maeneo ambayo yana hati iliyo hai kabla tarehe ya ukomo iliyowekwa, na wanasaidiwa katika kurejesha njia zao za kujikimu kimaisha. Mchakato huu unaongozwa na Sheria ya Tanzania pamoja na Viwango vya Mazingira na Jamii vya Benki ya Dunia Namba 5 (ESS5), na viwango vya ESS5 vitatumika kwanza inapotokea kuna viwango viwili vinatofautiana kuhusiana na taratibu hizo.
